**"ULEMAVU BARANI AFRIKA"**

**EPISODE 10: "Oluanda's story"**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**List of characters / Episode 10:**

**MSIMULIZI**

**SCENE ONE: LATE EVENING AT CHITOTO'S HOMESTEAD**

- Chitoto (mume, 18)
- BW. Mali (mume, 50)
- BI. Mali (mke, 45)
- Fagilio (mume, 42)

**SCENE TWO : KANGWA'S ROOM AT THE MALI HOUSE**

- BW. Mali (mume, 50)
- BI. Mali (mke, 45)

**SCENE THREE : AT OLUANDA'S PLACE**

- Kangwa (mke, 18)
- Oluanda (mume , 18)
  BW. Mali (mume ,50)
- BI. Mali (mume, 45)

**SCENE FOUR: NIGHT AT THE KAREMI'S HOME**

- Zabibu (mke, 15)
- Karemi (mume, 18)
- Theresa (mke, 65)

**SCENE FIVE: PEACEFUL MARCH AT MAGANYE**

- Chitoto (mume, 19)
- Oluanda (mume, 18)
- Leader (mume, 55)
- Umati ( wake na waume umri mchanganyiko)

**UTANGULIZI:**

Salamu nyingi na karibu katika kipindi cha Noa bongo,jenga maisha yako. Leo tunahitimisha kipindi chetu cha “ **Walemavu barani Afrika”.** Katika kipindi kilichopita, Chitoto aliharakishwa hospitali na Bw na Bi. Mali, ilipokuwa nusura wamvyoge kwa gari alipokuwa akivuka barabara akiwa mlevi chakari. Kwengineko, jukwaa likiwa tayari limeandaliwa kuadhimisha maandamano ya amani kupigania haki za walemavu wa Maganye. Maandamano hayo yalithibitishwa na Inspekta Joe, ambaye alimkabidhi Oluanda na wenzake kibali hicho. Kaa nasi, tunapohitimisha kipindi hiki kwa isimu ya **“Hadithi ya Oluanda”.** Tujiunge na Bw na Bi.Mali wakimregesha Chitoto nyumbani kwao, baada ya kufanyiwa uchunguzi na Dkt. Esther kule hospitali.

**SCENE ONE : LATE EVENING AT FAGILIO’S HOMESTEAD**

1. **SFX:** **CAR COMES TO A STOP**

2. **SFX:** **AMBIENCE INSIDE A DRIVING CAR**

3. **BW.MALI:** Hapa sio? Una hakika hapa ndipo unapoishi?

4. **SFX:** **CAR BREAKS HEARD FROM INSIDE THE CAR**

5. **CHITOTO:** Ndio,ni hapa . Yule pale ni babangu.

6. **BI.MALI:** Mumewangu, nenda ukaseme nae, anaonekana ni mkali sana

7. **CHITOTO:** Ndio , tafadhali njoo umuelezee.

8. **SFX:** **CAR DOOR OPENS, EVENING AMBIENCE**

9. **BW.MALI:** Sawa,tufanye hivyo basi. Wacha tumalize haya turudi nyumbani tukichelewa sana Kangwa atashikwa na wasiwasi.

**10. SFX:** **STEPS OF TWO PEOPLE**

11. **FAGILIO:** **(Angry)** Chitoto! Ulikuwa wapi? Umewafanyaje hawa watu wakati huu?... **(Concerned)** Chitoto, Mbona una bandeji? Umefanyika nini?

12. **BW.MALI:** Wacha nikueleze mimi .

13. **MSIMULIZI:** Ni bahati; Hayo ndio maneno Dkt. Esther aliyosema, baada ya kumchunguza Chitoto. Akasema ana bahati hakupata jeraha lolote kubwa lakini angeligongwa na gari angelipoteza hata uhai wake au kumfanya mlemavu kama Oluanda. Na Bw. Mali alichukuwa muda wake kumueleza Fagilio kwamba ni ulevi wa Chitoto ndio ulisababisha ajali ile. Baada ya hayo Bw na Bi. Mali

walielekea kwao,Lakini wakifika kwao waliduwaa walipompata Kangwa ameadimika. La uchungu zaidi walikuta baadhi ya vitu vyake pia vimekosekana isipokuwa kijibarua kidogo kilichoandikiwa mamake, Bi. Mali. alikichukuwa mikono ikimtetema…

**SCENE TWO : KANGWA'S ROOM AT THE MALI HOUSE**

14. **BW. MALI:** Ifunguwe! Ni lazima tujuwe haraka Kangwa amefanyika nini.

15. **SFX:** **LETTER RIPPED OPEN..**
**(Mrs. Mali starts to read the letter)**

16. **BI.MALI:** **(Takes a deep breath, reads slowly)**
Kwa Baba na Mama. Musiwe na hofu na ni muhimu mutambuwe kuwa nimekuwa mtu mkubwa sasa na nahitaji hata kuishi peke yangu kwa sababu muda mwingi hata hivyo huwa siwaoni, kutoniona kwangu lisiwe tatizo kwenu. Baba, nashkuru kwa kila kitu. Mama nakupenda sana, naomba ungekuwa kama mamake Oluanda. Ni mkarimu, siwezi kuepuka kuwa mavyaa wake na nitaolewa na kijana wake. Tuonane kesho katika maandamano. Binti yenu mpendwa, Kangwa.

17. **MSIMULIZI:** Bi. Mali alihukumika,alipomaliza kuisoma barua yake. Alishukuru kuwa Kangwa yu salama, lakini alichomwa na maneno ya binti yake. Bw. Mali hakutaka kusema lolote. Tukirudi nyumbani kwa kina Oluanda.

**<u>SCENE THREE: AT OLUANDA'S PLACE</u>**

18. **SFX: BACKYARD AMBIENCE**

19. **OLUANDA:** Kangwa, huwezi kufanya hivi. Bado ni wazazi wako. Utahitajika kurudi. Isitoshe,huwezi kuishi hapa, utaongeza shida zaidi.

20. **KANGWA:** Oluanda, sitaki kuishi na mzazi ambaye ni mkaidi, asiye elewa kuwa walemavu pia ni watu…wana hisia kamili, wanaweza kupenda na kupendwa pia…

21. **OLUANDA:** Sikatai. Lakini juu ya yote, bado nakuuliza urudi nyumbani. Kutoroka sio suluhisho.

22. **MSIMULIZI:** Huku Oluanda akijaribu kumfahamisha Kangwa arudi nyumbani, Bw. Mali na Bi. Mali walifika pale, nyuso zao zilijaa huruma na aibu. Tujue walisema nini.

23. **BI. MALI:** **(Crying out)** Kangwa! Binti yangu mrembo.. kipenzi..!

24. **KANGWA:** Mama na Baba… munafanya nini hapa?

| | | |
|---|---|---|
| 25. | **BW. MALI:** | Mamako amesema hatapata usingizi mpaka akuone… ,amefanya kuniburuta kama gunia hadi hapa |
| 26. | **KANGWA:** | Oluanda, huyu hapa ni mamangu. Mulishakutana na babangu.. |
| 27. | **OLUANDA:** | Nashukuru nfurahii kukuona mama... |
| 28. | **BI. MALI:** | Nafurahi kukuona Oluanda. Kangwa tafadhali njoo tuseme na wewe kidogo… |
| 29. | **BW. MALI:** | Kama kawaida, maongezi ni ya wanawake, wanaume wanaachiwa kazi. Oluanda, wacha nikuarifu ni kina nani wanahudhuria kesho. **(Talks while leaving)** Hutaamini nakwambia… |
| 30. | **SFX:** | **LAUGHTER FROM OLUANDA AND MALI** |
| 31. | **BI. MALI:** | Kangwa, nilifikiria sana kuhusu uhusiano wako na Oluanda. Na ajali yetu ya leo imenipa mtazamo tofauti wa maisha. |
| 32. | **KANGWA:** | **(Shocked)** Ajali? Ajali gani mama? Uko salama? |
| 33. | **BI. MALI:** | Ndio, sote tu salama. Usiwe na wasiwasi, Nitakueleza kisha. Jambo ni kuwa, nilifanya makosa kusema maneno machafu kuhusu Oluanda.Na nimekuja kukwambia .. samahani. |

Kwa hivyo rudi nyumbani, Na kuanzia leo utaniona nikiwa tofuati.

34. **MSIMULIZI:**Wakati mama na binti yake wakila suluhu, kila nyumba katika kitongoji cha Maganye kilizungumzia maandamano ya walemavu yalioandaliwa na Oluanda. Moja ya nyumba hizo ni ya kina Karemi, ambapo Karemi, Zabibu na nyanya yao Theresa walikuwa wamekaa mezani.

**<u>SCENE FOUR: NIGHT AT THE KAREMI'S HOME</u>**

35. **SFX:** **NIGHT AMBIENCE**

36. **ZABIBU:** **Nyany**a Theresa, kila mtu hapa Maganye atakwenda maandamanoni. Labda pia mimi nipange maandamano ya mazeruzeru hapa Maganye.

37. **THERESA:** Zabibu,Wewe umchanga sana. Na pia hakuna mazeruzeru wengi hapa Maganye kama walivyo walemavu wengine.

38. **KAREMI:** Hiyo sio sababu ya kumzuia kuja maandamanoni. Hata yeye huhujumiwa kama walemavu wengine. Akijitokeza, atawawakilisha zeruzeru wengine.

39. **ZABIBU:** Haswa, nitavaa miwani ya jua, rinda refu, alafu nitaonekana kama mtalii.

**(They all laugh heartily)**

40. **THERESA:** Je, watu wakianza kukuchokoza? Wakikucheka na kukuita majina? Sitakubali hayo!

41. **ZABIBU:** Hawawezi! Kwanza hao watu hawatakiwi kuwa hapo. Maandamano haya yanapinga tabia hizo. Si ndio kaka?

42. **KAREMI:** Ndio, nitakuwa hapo kukuchunga. Atakayekuchokoza wewe amenichokoza mimi na familia yetu kwa ujumla.**(Serious tone)**

43. **THERESA:** Karemi, Ulipotamka maneno hayo, umenikumbusha kuhusu babako. Alikuwa akisema maneno yayo hayo kuhusu hali ya Zabibu. Sasa sina haja tena ya kumlinda Zabibu. Najua yuko salama mikononi mwako. kalaleni. Kesho mutahitaji nguvu kwenye maandamano.

44. **ZABIBU:** **(Screams in delight)** Ndiooooo!

45. **MSIMULIZI:**Usiku huo, wakati mishumaa na vibatari vya Maganye vikizima, kama ishara ya watu kuenda kualala, ilikuwa rahisi kuhisi furaha iliyotanda angani. Siku iliyofuata, kulikuwa kuna kongamano kubwa mno na sio tu Maganye bali nchi nzima . Viongozi wa upinzani, wakereketwa wa haki zakibinaadamu, jekejeke la wafanyikazi, wanahabari watakuwepo na kila mmoja wa mkaazi wa Maganye angeliwakilisha familia yake. Jumuiko hili lilishinda lile la mashindano ya magari la safari rali. Walemavu wote wa Maganye walikuweko wakiongozwa na

Oluanda, Kangwa, Gidi na amini usiamini.. Chitoto!

**SCENE FIVE: THE PEACEFUL MARCH AT MAGANYE**

**(LARGE CROWD CHANTING)**

46. **UMATI:** Tunataka haki zetu! Tunataka haki sawa!

**47. OLUANDA: (Addresses crowd from loud speaker)** Asanteni. Asanteni sana.Huu sio mkutano wa kisiasa. Ni maandamano ya amani kuieleza serikali yetu, viongozi wetu, ya kwamba, hata walemavu wanahitaji haki na nafasi sawa!

48. **SFX:** **HUGE APPLAUSE FROM CROWD**

**(CROWD KEEPS CHANTING)**

49. **UMATI:** Oluanda! Oluanda! Oluanda!

50. **OLUANDA:** Hili halinihusu mimi pekee;linamuhusu mlemavu yeyote aliyeko hapa, nyumbani,hospitali yeyote hapa nchini au nje ya nchi.nawashukuru kwa kuja na kutuunga mkono. Sasa tutampa fursa kiongozi wetu atuzungumzie kabla ya kuanza maandamano yetu ya amani.

51. **KIONGOZI:** Katika mikutano yote niliyokwenda kama mwanasiasa, sijawahi kuona umati mkubwa

kama huu natamani hizi zingelikuwa ni kura zangu mwakani!

52. **SFX:** **CROWD BREAKS INTO LAUGHTER**

**53.** **KIONGOZI:** Naomba kusema hivi. Tumesikia vilio vyenu. Tutaisukuma serikali tuweze kupitisha sheria mpya bungeni inayotetea haki za walemavu katika Nyanja zote za Maisha, iwe ni elimu, afya, jamii na hata kisiasa. Ni wakati tupate uwakilishi wa walemavu bungeni! Haki sawa kwa walemavu!!!

54. **UMATI:** **(Shouts)** Tunataka haki sawa!

55. **CHITOTO:** **(Whistling to Oluanda as they did before the accident)** Oluanda, sikulaumu ukinichukia kwa yote niliyokutendea...sistahili kuwa rafiki yako tena. Lakini,nisamehe naomba kutubu kwani karibu nipoteze maisha yangu.

56. **OLUANDA:** Chitoto, kupoteza mguu wangu kumenifunza mengi...mojawapo ni chuki ambayo humla mtu ndani kwa ndani kama saratani. Nilikusamehe kitambo. Hivyo ndivyo nilivyoepuka chuki na hukumu. Njoo, jiunge katika maandamano. Nataka kukutambulisha kwa marafiki wangu wapya.

**HITIMISHO:**

Kwa hayo, maandamano yalianza, wakiangaziwa na wanahabari, waliosimama hapa na pale kuchukuwa visa tofauti vya walemavu hao, kuhusu masaibu yao.maandamano yalipofikia mwisho, Oluanda alikuwa kipenzi cha wengi, na akaalikwa kuzungumza bungeni na vikao vyengine kuhusu sera za walemavu. Bw na Bi. Mali walibubujikwa na machozi walipomuona binti yao akiwajibika kikamilifu. Zabibu, Karemi na nyanya yao Theresa walikuwepo kuifanisha siku hii na kwa matamshi ya nyanya Theresa mwenyewe, “gudulia leo keshavunjwa”, walemavu leo na kuendelea hawatengwa tena. Na kwa hayo tunatamatisha hadithi yetu kwa jina, **“ Ulemavu barani Afrika”**.Mchezo huu uliandikwa na Chrispin Mwakideu. Kusikiliza tena kipindi hiki au chengine tembelea tovuti zetu,  www.dw-world.de/lbe.
Tutashukuru kupata maoni yako, tupe hisia zako na mguso wa kipindi hiki katika maisha yako. Mpaka tutakapo tandika jamvi jengine la riwaya nyengine, tunakutakia kila la heri.